YALIYOMO

DIBAJI iii

TABARUKU iv

SURA YA KWANZA 1

SURA YA PILI 12

SURA YA TATU 16

SURA YA NNE 23

SURA YA TANO 33

SURA YA SITA 39

SURA YA SABA 43

SURA YA NANE 48

SURA YA TISA 56

SURA YA KUMI 65

SURA YA KUMI NA MOJA 69

SURA YA KUMI NA MBILI 73

SURA YA KUMI NA TATU 76

SURA YA KUMI NA NNE 79

SURA YA KUMI NA TANO 82

SURA YA KUMI NA SITA 89

SURA YA KUMI NA SABA 98

SURA YA KUMI NA NANE 107

SURA YA KUMI NA TISA 115
SURA YA ISHIRINI 122
SURA YA ISHIRINI NA MOJA 130

DIBAJI

Riwaya hii ya *Nyumba Yangu, Machozi Yangu* ni simulizi ya kusisimua, ya huzuni, matumaini na ushindi. Inaangazia maisha ya Mama Kanje, mwanamke aliyepitia mateso mengi – kutoka vita vya Rwanda, maisha ya kambi ya wakimbizi, manyanyaso ya ndoa, hadi mapambano ya kutafuta maisha bora kwa ajili ya watoto wake. Hii ni hadithi ya ujasiri wa mwanamke anayeamka kila siku na kupigana na dunia kwa ajili ya familia yake. Ni sauti ya wanawake wote waliotelekezwa, waliopigwa, waliolilia haki zao kimya kimya. Hadithi hii inalenga kuibua hisia, kuleta hamasa, na kutoa tumaini kwamba hata giza nene linaweza kuwa na mwisho wa mwanga.

TABARUKU

Naandika riwaya hii kama sadaka ya moyo wangu kwa wanawake wote waliopitia magumu ya maisha, waliokosa msaada, waliolia kimya kimya usiku wa manane, lakini hawakukata tamaa.

Mama Kanje ni ishara ya mwanamke jasiri, mama shujaa, aliyeamua kufa maskini lakini akiwa na heshima. Nawadu kazi hii kwa mama yangu, kwa wanawake wa Afrika, na kwa vizazi vijavyo vya mabinti watakaojifunza kupitia kalamu hii kuwa mateso si mwisho wa hadithi. Hii ni hadithi ya maisha, na maisha ni hadithi isiyoisha…

Ninawashukuru SOMA kwa kuniwezesha kujiunga na mpango wa mentorship ulionikutanisha na Anna Mbise, ambaye alinishauri kuandika kitabu changu. Pia,

nawashukuru familia yangu, hasa mama mzazi, kwa kuniombea kila siku. Vilevile, nawashukuru rafiki yangu wa karibu Zaituni Ally kwa kunisapoti katika mawazo yangu na kunipa amani ya moyo kila wakati.

SURA YA KWANZA

Ilikuwa siku mbaya sana kwa Mama Kanje katika biashara yake ya kuuza ndizi sukari, siku hiyo y a juma mosi alitoka sokoni mapema kwasababu nyumbani alikuwa anauguza mtoto, alilazimika kufunga biashara yake mapema kabla ya muda bila hata kumaliza mzigo wake.

“Nimesema tokeni kwenye nyumba yangu, tokeni haraka sana! Hauna hata aibu mwanaume wewe! Unawezaje kuniletea mwanamke mwingine kwenye nyumba yangu? Huoni aibu hata mbele za watoto wako unawafundisha nini sasa, nimesema tokeni haraka kabla sijachinja mtu hapa!”

Ni maneno ambayo aliyasema Mama Kanje kwa hasira huku machozi yakimtiririka kwa uchungu

baada ya kumkuta mume wake ameketi sebuleni na mwanamke mwingine baada ya kutoka sokoni.

Haikuwa mara ya kwanza kwa Mama Kanje kufanyiwa vituko na ukatili na mumewe, yote yalianza mara baada ya familia hiyo kupata mtoto wao wa kwanza mwaka 1998.

Kupigwa, kutukanwa mbele za watu halikuwa jambo la kushangaza kwa Mama Kanje, hakuwa na pakukimbilia kwasababu hakuwa na ndugu yeyote wadamu! Ambapo angekimbilia kuyakwepa mateso na manyanyaso kutoka kwa Baba Kanje.

****

Mama Kanje alizaliwa mwaka 1983 katika nchi ya Rwanda, alibahatika kusoma mpaka darasa la pili na hakuweza kuendelea na masomo tena kwasababu ya ugumu wa maisha, katika familia

yao walikuwa Watoto watatu, yeye akiwa mtoto wa kwanza.

Msiba ulianzia siku ya vita ya Wahutu na Watutsi mwaka 1994 ambayo hatakuja kuisahau kwani ilimfanya aishi kama yatima asiye na uhakika na uyatima wake!

Siku chache kabla ya vita Mama Kanje alikwenda kumtembelea Shangazi yake aliye kuwa anakaa Kijiji tofauti na Kijiji walichokuwa wanakaa yeye na wazazi wake, baada ya siku mbili aliamua kurudi nyumbani.

Mama Kanje akiwa njiani kurudi kijijini kwao alisikia milio ya bunduki na mabomu! Hakuweza kuendelea na safari yake ya kurudi nyumbani bali alianza kukimbia kwa uoga mkubwa sana kwani kwa wakati huo alikuwa mdogo sana mwenye umri wa miaka 11 tu.

Siku hiyo ndipo Mama Kanje alipopotezana na familia na ndugu zake wote, hakujua kama wamekufa au wako hai, katika kukimbia Mama Kanje alikutana na kundi la watu wengine wanaokimbia akaamua kukimbia nao, walikimbia mchana kutwa bila kula chochote, usiku walijificha vichakani kuhofia kukutana na wauwaji, maisha yakawa magumu sana, kuna wakati walilazimika kula mahindi mabichi!

Kwasababu ya njaa kali hapakuwa na muda wa kupika maporini, zaidi ya kukimbilia mpakani mwa Rwanda na Tanzania kupata msaada.

Walifanikiwa kuvuka mpakani Rusumo Tanzania wakiwa salama na wakapelekwa katika kambi ya wakimbizi Rumasi iliyokuwa wilaya ya Ngara mkoani Kagera.

Mama Kanje alijisajiri kama mtoto katika familia nyingine ambayo alikimbia nayo, hapo walipewa chakula kulingana na idadi yao lakini aliishi kwa taabu sana kwani kuna wakati familia hiyo walimgawia chakula kidogo sana, walimtenga na kuna siku hakupewa hata kidogo akalala njaa.

Siku moja Mama kanje alikwenda kuchota maji kisimani kambini, akapata Bahati ya kukutana na mtu ambaye alikuwa anafahamiana na wazazi wake, alikuwa ni Jirani yao kule nyumbani Rwanda, akafurahi sana kwani angekuwa kama ndugu yake pekee anayejuana naye, alimuelekeza anapokaa kambini humo na Mama kanje akajisemea

“Nitakwenda kuwaaga pale ninapokaa halafu nitakuja kukaa na huyu Jirani yangu angalua nitapata maisha mazuri”.

Waliagana vizuri na Mama Kanje akarudi nyumbani akawaeleza kuwa amepata ndugu yake na ataondoka Kwenda kwake.

Familia hiyo hawakufurahia kabisa jambo hilo kwani kupungua kwake kungepunguza idadi na wingi wa chakula walichokuwa wakigawiwa.

Hatimaye ulifika muda wa Mama Kanje kuondoka na aliwaaga familia hiyo waliokuwa kama walezi wake kwa muda mfupi, kwa Bahati mbaya sana Mama kanje baada ya Kwenda kwa yule ndugu yake aliyekutana naye kisimani hakumkuta!

Alikuwa tayari ameshahamishwa Kwenda kambi nyingine kwani kambi hiyo ilikuwa imejaa, wakati wanapunguza watu Kwenda kambi nyingine, ndugu huyo naye akahamishwa, Mama Kanje alijiskia vibaya sana na hakuwa na chaguo

lingine zaidi ya kurudi kule kwa ndugu walezi. Kwao walifurahia kwani kuwepo kwake ilikuwa inaongeza kushiba kwao.

Mama Kanje alichukuliwa na familia nyingine kutoka kambini, kwani kulikuwa na utaratibu watu kutoka maeneo mbalimbali ya Tanzania, walifika kambini na kuomba kupewa wakimbizi kwaajili ya kuwasaidia na kuishi nao.

Mama Kanje nayeye alichukuliwa na mzee aliyejulikana kwa jina la Mtuku, hapo Mama Kanje akapata furaha sana kwakuwa alitarajia kupata maisha mazuri na kupumzika manyanyaso aliyokuwa akipata akiwa kambini, lakini haikuwa hivyo, Mzee Mtuku alikuwa anaishi na mkewe na hawakubahatika kupata mtoto, walikuwa wanaishi Kijiji kinachoitwa Kona-9.

Mama Kanje akawa mtoto mpya katika familia hiyo japo hakuishi kama mtoto bali kama mfanyakazi asiyekuwa na mshahara.

Familia hiyo ilimchukuwa Mama Kanje kwalengo la kumfanyisha kazi wala sio kumsaidia kwani walimtuma sehemu za mbali sana kupeleka ndizi tena bila usafiri, alibeba mkungu wa ndizi kichwani na kutembea umbali mrefu sana

Familia ya Mzee Mtuku hawakumpatia hata chakula wala maji ya kunywa akiwa njiani, Mama Kanje hakuwa na chaguo zaidi ya kufanya kazi ngumu zilizoshinda umri wake, alilazimika kutoka Kijiji cha Kona-9 mpaka Kijiji cha Mmiterama umbali wa takribani kilomita 35 huku akiwa na mkungu wa ndizi kichwani, njiani alipumzika kidogo kish angeendelea na safari mpaka afikishe mzigo, na baada ya kufikisha

mzigo alipumzika siku moja tu baada yah apo alilazimika kurudi nyumbani na pesa alizopewa huko alikopeleka ndizi.

Maisha yaliendelea kuwa magumu sana kwa Mama Kanje, akakonda sana na kuna wakati aliugua sana lakini lakini hakupata msaada zaidi ya kutukanwa na Mzee Mtuku,

“Najua hauna ugonjwa wowote unakwepa tu kazi, sasa nakwambia uchague mwenyewe kati ya kupeleka mzigo au kurudi kambini, sisi siyo wazazi wako ala!”

maneno hayo aliyazungumza Mzee Mtuku kwa hasira baada ya Mama Kanje kusema kuwa anaumwa hawezi kubeba mzigo umbali mrefu. Lakini hakuwa na lakufanya alibeba mzigo kukamilisha ratiba yake, akiwa njiani alizidiwa akashindwa kuendelea na safari, alitokea

msamaria mwema akamsaidia, akampeleka mpaka nyumbani kwake katika Kijiji cha Mrukulazo.

Mama Kanje baada ya kupata msaada hakutaka tena kurudi nyumbani kwa Mzee Mtuku maana angeona cha mtema kuni kupoteza mzigo njiani.

Mrukulazo yakawa makazi mapya kwa Mama Kanje, hapo aliishi bila mateso na alilelewa kama Watoto wengine katka familia hiyo mpya.

Baada ya muda kupita Mama Kanje aliugua ugonjwa wa akili, usiku aliamka na kuanza kuondoka akidai kuwa kuna mtu anamuita, hali hiyo ilisababishwa na msongo wa Mawazo akiwakumbuka wazazi wake na ndugu zake waliopotezana vitani. Mama wa familia hiyo mpya ya Mrukulazo aliamua kumpeleka Mama Kanje kwa dada yake ambaye alikuwa anakaa

Kijiji cha Msumba ambapo ilikuwa rahisi kupeleka Mama Kanje Kanisani kupata huduma ya maombi.

Hapo Msumba alikaa katika familia ya Bibi na Bwana John ambapo aliishi bila kuteswa na alikuwa kama mtoto wa familia akawa dada wa Watoto wa familia hiyo, hapo alijifunza ujuzi wa kufuma mikeka kwa kutumia majani na aliweza kuuza na kupata fedha za kumudu mahitaji yake, pia alijifunza kutengeneza pombe za kienyeji ikamuongezea kipato na kuweza kumudu maitaji kama kujinunulia nguo.

SURA YA PILI

Mwaka 1997 Mama Kanje akiwa na umri wa miaka kumi na nne tu aliolewa, kulingana na hali ya maisha ya wakati huo Aliona ni kama Bahati kumpata mume na familia ya John wakampa baraka na kumruhusu akaanzishe maisha na Mr. Mibulo.

Mr. Mibulo alikuwa fundi wa kujenga nyumba na mkulima pia. Walianza kuishi Pamoja kwa furaha katika nyumba yao iliyoezekwa kwa Majani makavu ya migomba na ukuta uliokandikwa kwa udongo katika Kijiji cha Murugwanza, kitongoji cha Mkanywampezi.

Furaha hiyo haikudumu na mwaka mmoja tu furaha na amani kwa Mama Kanje vikawa hadidhi ya kusadikika! Walipata mtoto wao wa kwanza mwaka 1998 na wakampa jina la kikabila Kanje lenye maana ya “Wangu”. Kuzaliwa kwa

Kanje ilikuwa ndio mwanzo wa mateso katika nyumba ya wawili hao.

Mtaji wa Mama Kanje uliisha wote katika matumizi ya nyumbani na mumewe, kuna wakati mumewe aliwaalika marafiki zake waje nyumbani kunywa pombe bila kulipa chochote na ikapelekea mtaji wote kuisha wakabati kutegemea kilimo tu.

Baba Kanje yeye alikuwa anapata vibarua vya kujenga nyumba lakini pesa yake ilikuwa kwajili ya kupendeza mwenyewe na kunywa pombe asikumbuke kuleta kitu nyumbani, alimnunulia Mama Kanje mafuta madogo ya kupaka ya shilingi mia tatu huku yeye akijinunulia mafuta mazuri na Marashi mazuri sana.

Siku moja Mama Kanje alitumia Marashi ya mumewe akakiona cha mtema kuni baada ya

Baba Kanje kurudi kutoka kazini na kukuta harufu chumbani, alimpiga sana kipigo cha mwizi!

“Shenzi kabisa wewe, unajua bei ya haya Marashi wewe? Unaweza kuyanunua wewe? Unataka unukie vizuri nani akutamani mbwa wewe? Leo nitakufundisha adabu ujue kuheshimu vitu vyangu”,

Maneno hayo aliyasema Baba Kanje huku akifoka na kumpa kipigo kikali Mama Kanje bila kumuonea huruma.

Majirani wote wa mtaa huo waliokuja nyumbani kwa Mama Kanje kumuulizia mumewe, hawakujisumbua kutambua kama Baba Kanje yupo au hayupo, sauti ya redio ndio ilikuwa ishara ya uwepo wa Baba Kanje kwani redio yake hakuruhusiwa kuwasha mke wake isipokuwa yeye mwenyewe, kwahiyo majirani wakisikia

muziki wa redio walitambua moja kwa moja Baba Kanje yupo na wasiposikia redio basi ilikuwa ishara tosha kuwa Baba Kanje hakuwepo Nyumbani.

SURA YA TATU

Mwaka mmoja baadaye walipata mtoto mwingine wapili wakampatia jina la Sembo, mzigo wa kulea watoto ukaongezeka kwa mama Kanje.

Chakula haikuwa tatizo sana kwa familia kwasababu Mama Kanje alikuwa anajitahidi sana kulima japo wakati mwingine mavuno hayo hayo yalibebwa na Baba Kanje na kuyauza ili wapate mahitaji mengine yaani sabuni, chumvi na mengine madogo madogo.

Wakati mwingine walikula chakula kisichokuwa na chumvi, hapo ilikuwa baada ya kuzunguka kwa majirani wote kuomba chumvi na baada ya kumaliza majirani wote basi waliamua kula chakula kisicho na Ladha ya chumvi.

“Huyu baba Kanje leo lazima nimkomeshe” Mama Kanje alijisemea baada ya kutoka kuomba chumvi kwa Jirani wan ne, alipika magimbi na maharage na akatia mchuzi lakini hakutia ile chumvi aliyoomba kwa Jirani, alipakua chakula kidogo akala kisha akapakua chakula kingine na kuweka kwenye bakuli ya chuma iliyokuwa nyeusi kwa ukuu wake, akahifadhi kwaajili ya mumewe.

“Leo nitaona kama ataweza kula chakula bila chumvi, labda atapata uchungu ajifunze kuleta chumvi nyumbani” Mama Kanje aliweka mtego kwa maksudi akamuwekea chakula bila chumvi.

Lakini wapi! Baba Kanje alikuwa na roho ngumu sana, alipofika nyumbani na kupewa chakula, alikula chote hakubakisha hata mchuzi, wala

hakuulizia chumvi na wala hakusema neno lolote na wala hakutoa hela ya chumvi bado!

Pesa nyingine Baba Kanje alitumia kununua pombe mpaka mazao ndani yaishe, Mama Kanje alikuwa Mjanja akakumbuka kuficha mbegu za mazao kwajili ya msimu mwingine.

Mama Kanje alipoona hali inakuwa mbaya zaidi nyumbani, aliamua kuanza kufanya biashara ya kuuza ndizi sukari na parachichi ili kupata mahitaji ya familia akauvaa ubaba licha ya kuwa na mume.

Hali ilikuwa mbaya zaidi pale ambapo Baba Kanje alianza kuchepuka na wanawake wengine tena bila kujificha. Siku moja Mama Kanje akiwa ameenda sokoni ktafuta riziki kupitia biashara, Baba Kanje alimteta Mwanamke nyumbani kwa Mama Kanje, hakuogopa watoto maana

walikuwa wadogo sana. Mama Kanje baada ya kutoka sokoni hakuamini macho yake baada ya kukuta kinachoendelea kati ya mume wake na mchepuko tena nyumbani kwake!

Hapo Mama Kanje hakuwa mnyonge, alinoa panga!

Baba Kanje na mchepuko wake wakaondoka na kumuacha Mama Kanje akilia bila kujua afanye nini, kwani hakuweza hata kufikiria kuondoka nyumbani.

******

Mwaka 2002, Mama Kanje akiwa mjamzito wa miezi nane, siku hiyo mume wake alirudi usku sana akiwa amelewa sana,

“We mkimbizi nifungulie mlango" Baba Kanje alisikika akiwa amekaribia kufika nyumbani”

“Nimesema fungua mlango, nitaingia na mlango ohooo!!"

Mlango ulipigwa teke hata kabla ya Mama Kanje kufika kuufungua, Baba Kanje baada kuingia ndani alimpiga teke la tumbo mke wake akadondoka kwenye meza yao ndogo ya mbao zilizo chakaa.

Alilia sana kwa maumivu huku akiwa ameshikilia tumbo lake kwa maumivu ya kipigo kwa kuchelewa kufungua mlango. Asubuhi Mama Kanje alipatwa na uchungu wa kujifungua kabla ya muda! Alimuomba Baba Kanje ampeleke hospitali lakini alijibiwa kwa maneno makali

“Yaani niache kazi zangu za maana eti nkupeleke hospitali!”

“Njia ya kwenda umeisahau? Mbona mimba ya kwanza ulijipeleka?”

“Hebu chukua hii miatano na nataka chenji irudi hujui zinavotafutwa”

Baba Kanje alimrushia shilingi miatano kisha akaondoka bila kujali hali ya mkewe.

Mama Kanje aliamua kutembea kwa miguu huku mgongani amembeba Sembo ambaye alikuwa ana miaka miwili, kutokana na umbali wa hospitali, maumivu ya uchungu na mzigo wa mtoto mgongoni Mama Kanje hakuweza kufika kufika hospitali!

Alijilaza kando ya barabara chini ya muembe ili kujikinga na jua kali na hapo alipoteza fahamu.

Kwa bahati nzuri wapita njia waliwahi kutoa msaada wakamchukua yeye na mtoto wake Sembo wakamuwahisha hospitali ya Murugwanza.

“Pole sana Mama”

Daktari alimwambia Mama Kanje.

“Inaonekana ulibeba mzigo mzito sana na pia ulifanya kazi ngumu ambazo zimepelekea kuwapoteza mapacha”.

Kumbe Mama Kanje alikuwa na mimba ya mapacha na wote walifariki, Mama Kanje hakuthubutu kusema kilichotokea jana yake usiku kwani kipigo kikali alichopata ndicho kilipelekea msiba, alilia sana kwa uchungu.

SURA YA NNE

Maisha ya Mama Kanje yaliingia katika giza nene baada ya kupoteza mapacha wake kutokana na kipigo cha mumewe. Hakuna aliyejua machungu aliyokuwa anayapitia, moyo wake ulibeba huzuni, hasira na upweke usioelezeka.

Alihisi dunia nzima imegeuka dhidi yake. Wakati mwingine alikuwa akikaa kimya kwa saa nzima, machozi yakimtiririka bila sauti.

Aliwatazama watoto wake wawili waliobaki kwa macho ya huruma, akijua kuwa hana mtu wa kumtegemea zaidi yao.

Baba Kanje hakujali kabisa, aliendelea na maisha yake kama hakuna kilichotokea. Hata baada ya kuzikwa kwa mapacha, hakuwahi kumwambia Mama Kanje neno la faraja. Badala yake alianza

kumleta waziwazi mwanamke mwingine nyumbani.

Mama Kanje aliamua kuvumilia kwa ajili ya watoto wake. Lakini kilichofuata kilimvunja kabisa moyo wake.

****

Siku ya Mama Kanje kufukuzwa nyumbani kwake ilikuwa kama kaburi linalomzika akiwa hai. Akiwa njiani kutoka kanisani siku ya jumapili, rafiki yake aliyeitwa Mama Ovoni alimwambia Mama Kanje,

“Baba Ovani ameniambia kuwa wakati anapiga stori na mume wako, alimsikia akisisitiza kuwa haogopi kumuua!”

Baba Kanje alisikika akisema,

“Hata Watanzania wanauawa, muuaji anafungwa baadaye anaachiwa, sembuse yule mkimbizi!?”

Ilionekana Dhahiri kwamba Baba Kanje hakuwa na mpango mzuri juu ya maisha ya mkewe.

Hakuna kilichoandikwa usoni pa Baba Kanje, wala huruma yoyote iliyosikika kwenye sauti yake.

“Ondoka! Nenda ukale jasho lako la ndizi na maparachichi. Hapa siyo kwako tena!” maneno hayo yalimchoma Mama Kanje kuliko kisu chenye ncha kali.

Watoto, Kanje na Sembo, walisimama mlangoni wakiwa kimya, macho yao yakiwa yamejaa machozi na hofu. Walitaka kumkimbilia mama yao lakini walishasomewa sheria mpya—wasithubutu!

Usiku huo, mvua ilinyesha kama ya maombolezo. Mama Kanje akiwa hana pa kwenda, alilazimika kulala kwenye stoo ya jirani aliyemhurumia. Alikuwa na nguo chache kwenye mkoba wake wa plastiki, na moyo wake ulikuwa umevunjika vipande vipande. Siku iliyofuata, aliamka mapema. Alichukua mtungi wa maji wa jirani, akajiosha kwa baridi kali. Hakujua pa kwenda, lakini alijua jambo moja

“lazima niishi kwa ajili ya watoto wangu”

Katika giza hilo, aliwaza kuhusu Kanje na Sembo, watoto wake waliobaki. “Je, wataishi bila mama yao? Je, nitawapata tena?” alijiuliza kwa sauti ya chini, huku baridi ikimudu kama kisu.

Alitembea hadi stendi ya basi ya Karagwe, akichukua gari na pesa chache alizokuwa ameweka akiba kutoka kwa biashara yake ya

ndizi. Njiani, alikumbuka maisha yake ya utotoni Rwanda—milipuko ya mabomu, wazazi wake waliopotea, na ndugu zake ambao hakuwa amewaona tangu vita vya 1994.

Alisema kwa moyo wake huku ameshika tama, “Maisha yamenitesa, lakini sitakata tamaa. Watoto wangu ni sababu yangu ya kuishi sina tumaini lingine tena.”

Karagwe ilikuwa tofauti na kijiji chake cha Murugwanza. Mji huo ulikuwa na hewa baridi, miti mirefu ya mvule, na nyumba za mawe zilizopakwa rangi ya manjano na kijani. Lakini baridi ya Karagwe haikuweza kumudu baridi ya moyo wake. Alipata kazi ya kuwa mtumishi wa nyumba kwa Bi. Kokuhumuliza, mama mkubwa mwenye watoto watano.

Kazi ilianza saa kumi alfajiri licha ya kulala saa sita usiku, alifanya kazi bila kupumzika, kufua nguo, kupika wali wa nazi, kusafisha vyombo, na kumudu kila amri ya watoto wa Bi.Kokuhumuliza.

"Wewe mkimbizi, kazi yako ni kuhakikisha kila kitu kiko sawa!"

Bi.Koku alisema kwa sauti ya kejeli siku moja. Mama Kanje alinyamaza, lakini moyo wake ulilia.

Kila jioni, baada ya kazi, aliketi chini ya mti wa mwembe karibu na nyumba, akichora jina la watoto wake kwenye mchanga (Kanje, Sembo). Alikumbuka tabasamu la Sembo alipomudu kuimba, na jinsi Kanje alivyopenda kuchora picha za ndege na nyota.

******

Alipata barua kutoka kwa jirani yao, Mama Ovoni, ambayo ilimudu machozi. Barua ilisema: “Kanje ana njaa, Baba Kanje ameshaoa mwanamke mwingine anaitwa Acsa, anawafungia ndani ya banda la kuni. Sembo ana homa mara kwa mara.”

Mama Kanje alisoma barua hiyo mara tatu, kila mara akiifuta machozi kwa khanga yake chakavu.

Hata hivyo, hakukata tamaa. Alipata rafiki mpya, Mama Zawadi, ambaye alikuwa anauza vitumbua karibu na soko la Karagwe, alionana naye pindi alipokwenda sokoni kununua mboga na vitu vingine alivyoagizwa na Bi.Koku kila siku ya jumamosi.

Mama Zawadi alimudu tabasamu la kwanza la Mama Kanje katika miezi mingi.

“Wewe ni mwanamke wa nguvu, Mama Kanje. Usiruhusu maisha yakushinde,” alisema Mama Zawadi.

Alimpa mkopo wa shilingi elfu kumi ili aanze kuuza ndizi tena siku za Jumapili. Mama Kanje aliweka pesa hizo kwa makini, akijua kwamba kila senti ilikuwa hatua kuelekea kumudu maisha ya watoto wake.

Bi. Kokuhumuliza hakumpa Mama Kanje siku ya kupumzika, isipokuwa jumapili tu, Mama Kanje alijitahidi kuwahi asubuhi sana, alipita sokoni kununua mzigo mdogo wan dizi kabla ya Kwenda kanisani, kisha alihifadhi kwa rafiki yake Mama Zawadi. Baada ya kutoka kanisani majira ya saa nne asubuhi alichukua mzigo wake wan dizi na kuanza kutembeza mpaka amalize. Baada ya kumaliza mzigo alirudi nyumbani kwa Bi.koku kabla haijazidi saa kumi alasiri. Ikitokea

hajamaliza mzigo, alilazimika kumuomba Mama Zawadi amsaidie kuuza, kwani ilikuwa ni mwiko kupeleka vifurushi vya ndizi kwa Bi.Koku.

Siku moja, akiwa sokoni, alisikia wimbo wa kanisani ukiimbwa na kwaya ya watoto. Wimbo huo ulimkumbusha nyimbo ambazo Sembo alikuwa akiimba nyumbani. Alisimama pembeni, akafumba macho, na kuomba:

"Mungu, nipe nguvu. Sitawaacha watoto wangu."

Alipofungua macho, aliona mwanamke mzee akiuza mikeka ya majani. Alimudu wazo: angeweza kuongeza ujuzi wa kufuma mikeka na kuuza ili kuongeza kipato. Alimudu siku moja ya mafunzo na mwanamke huyo kwakuwa alikuwa tayari ana ujuzi wa awali aliojifunza kabla hajaolewa kwa Baba Kanje, na akaanza kufuma

mikeka kila jioni baada ya kazi. Alifanya kazi zake kwa bidi ili apate muda jioni wa kufuma mikeka bila kugombezwa na Bi. Kokuhumuliza.

Kwa muda mfupi tu, Mama Kanje alikuwa ameanza kuona mwanga mdogo katika giza lake. Alikuwa na mkopo wa kuuza ndizi, na alikuwa ameanza kufuma mikeka. Lakini bado alikuwa mbali na watoto wake, na moyo wake ulibeba uzito wa upweke. Aliahidi moyoni:

“Siku moja, nitawarudishia watoto wangu tabasamu lao.”

SURA YA TANO

Mama Kanje aliendelea na kazi yake ya ndani huku akiuza ndizi na mikeka siku za Jumapili. Maisha yake yalikuwa kama vita vya kila siku, lakini kila jasho alilotoa lilikuwa na maana—watoto wake. Alipata barua nyingine kutoka kwa Mama Ovoni, ambayo ilimudu habari za Kanje na Sembo.

Kanje alikuwa ameanza kuonyesha ukaidi shuleni, akijaribu kujilinda dhidi ya kejeli za watoto wengine waliomwita “mtoto wa mkimbizi.” Sembo, kwa upande mwingine, alikuwa akionyesha talanta ya uchoraji, lakini mara nyingi alikuwa akilala darasani kwa njaa.

Mama Kanje alihisi kama moyo wake unavunjika vipande vipande. Alikumbuka siku alipowabeba watoto wake mgongoni, akiwaimbia nyimbo za Rwanda za utulivu. Aliketi jikoni usiku mmoja,

akiangalia taa ya mshumaa ikiyeyuka polepole. “Je, nimewatelekeza watoto wangu?” alijiuliza. Lakini akajikumbusha:

“Sio kosa langu. Ninapambana kwa ajili yao.”

Alipata wazo la kuongeza bidhaa zake za kuuza. Mbali na ndizi na mikeka, alianza kufuma vikapu vidogo vya kumudu vyombo vya jikoni.

Alipata wazo hili baada ya kuona jirani yake, Mama Zawadi, akiuza vikapu sokoni. Alimuomba Mama Zawadi siku moja ya mafunzo ya ziada, na akaanza kufuma vikapu usiku baada ya kazi.

Vikapu hivyo vilianza kumudu wateja, hasa akina mama waliopenda muundo wake wa kipekee uliokumbusha miundo ya Rwanda.

******

Siku moja, alipokea mwaliko wa kuhudhuria mkutano wa wanawake wa Karagwe waliokuwa wakijishughulisha na biashara ndogo ndogo.

Aliomba ruhusa kwa Bi.Kokuhumuliza na aliruhusiwa japo kwa mashariti.

“Lazima hii siku nitaikata kwenye mshahara wako, hakuna pesa za bure hapa” Bi. Kokuhumuliza alisema.

Mkutano huo ulikuwa wa kwanza kwake, na alihisi hofu ya kuingia katika chumba kilichojaa wanawake waliovaa vitenge vya rangi nzuri na za kupendeza, yeye alikuwa na khanga yake moja aliyotoka nayo Ngara, lakini hakuwa muoga katika hili.

Lakini alipotambulishwa na Mama Zawadi kama “Mama Kanje, mwanamke wa nguvu,” alihisi heshima ndani yake ikirudi. Alishiriki hadithi

yake ya maisha, japo kwa aibu, na akagundua kuwa wanawake wengi walikuwa wamepitia mateso kama yake. Mkutano huo ulimudu nguvu mpya ya kuendelea.

Aliporudi nyumbani, alipata barua nyingine kutoka kijijini. Ilisema kuwa Acsa alikuwa amezidi kuwatesa watoto wake, akiwafungia ndani ya banda la kuni kwa masaa mengi. Mama Kanje alilia usiku huo, lakini badala ya kukata tamaa, aliamua kuongeza juhudi zake.

Alituma pesa kidogo aliyokuwa ameweka akiba kwa jirani, akiomba awanunulie Kanje daftari na kalamu, na Sembo viatu vya shule.

“Hata kama siko nao, watajua mama yao anawapenda,” alisema kwa moyo wake.

Mama Kanje alikuwa tayari amejifunza jinsi ya kuwa na marafiki wa kuaminika. Mama Zawadi

alikua kama dada yake, akimshauri jinsi ya kuongeza wateja wa biashara yake.

Alimudu pia wazo la kuanzisha kikundi kidogo cha wanawake wa Karagwe waliokuwa wakifanya kazi za ndani, ili waweze kuweka akiba pamoja. Kikundi hicho kilianza na wanawake watano, wakiweka shilingi elfu moja kila wiki. Mama Kanje alihisi kana kwamba alikuwa akianza kujenga daraja kuelekea maisha bora.

Mama Kanje alipokea picha ndogo iliyotumwa na jirani—picha ya Kanje na Sembo wakiwa wamesimama mbele ya shule yao, wakiwa wamevaa jezi za rangi ya manjano. Alishika picha hiyo kwa mikono miwili, akaiweka karibu na moyo wake, na kusema:

“Hivi ndivyo maisha yanapaswa kuwa. Watoto wangu watajua furaha siku moja.”

SURA YA SITA

Mama Kanje aliendelea na kazi yake ya ndani huku akiuza ndizi, mikeka, na vikapu siku za Jumapili. Alikuwa ameanza kupata wateja wa kawaida sokoni, ambao walimudu tabasamu la heshima.

Lakini maisha yake bado yalikuwa magumu. Bi. Kokuhumuliza alikuwa akimpa kazi za ziada, kama kufua nguo za majirani, na mara nyingi alilazimika kula chakula kidogo cha mabaki.

“Unakula chakula cha watoto wangu, ni nini hujui aibu?” Bi. Fatuma alisema siku moja.

Mama Kanje alinyamaza, lakini moyo wake ulijawa na hasira ya kimya.

Usiku mmoja, alipokuwa akifuma kikapu chini ya taa ya mafuta, alisikia sauti ya mvua ikinyesha nje. Sauti hiyo ilimkumbusha usiku alipofukuzwa na

Baba Kanje. Alifunga kikapu chake, akachukua daftari lake dogo, na kuandika:

“Maisha yangu ni kama mvua hii—ina baridi, lakini inaisha. Nitapata jua langu siku moja.” Alipata nguvu ya kuendelea kutokana na maneno yake mwenyewe.

Alipata fursa ya kuhamia Bukoba kwa dada wa Bi. Kokuhumuliza, Bi. Melisa, ambaye alikuwa na nyumba kubwa ya ghorofa mbili.

Bi. Melisa alikuwa tofauti kidogo—alimpa Mama Kanje siku moja ya mapumziko kwa mwezi na alimruhusu kutuma barua kwa watoto wake.

Huko Bukoba, Mama Kanje alipata fursa ya kuendelea na biashara yake ya mikeka na vikapu, na akaanza kuuza vitumbua asubuhi kabla ya kazi.

Alipata wateja wapya, wengi wao wakiwa wafanyakazi wa ofisi za serikali karibu na soko.

Siku moja, alikutana na mwalimu wa shule ya msingi, Bwana Yusuph, ambaye alimwambia kuhusu mpango wa kusaidia watoto wa wakimbizi kupata elimu.

“Unaweza kuwasilisha maombi kwa ajili ya watoto wako,” alisema Bwana Yusuph.

Mama Kanje alishukuru, lakini alijua kuwa bado alikuwa mbali na kumudu ada za shule. Alichukua fomu za maombi na kuziweka chini ya godoro lake, akiwa na matumaini ya siku moja kuzisajili.

Mama Kanje alianza kujifunza kuhusu umuhimu wa elimu kwa watoto wake. Alipata barua nyingine kutoka kijijini, ikisema kuwa Kanje alikuwa ameanza kuongoza darasani licha ya

mateso ya Acsa. Sembo alikuwa ameanza kuchora picha za miti na nyota, na alimuandikia Mama Kanje barua fupi:

“Mama, ninakukumbuka. Ninapenda kuchora kama ulivyoniambia kuhusu Rwanda.” Barua hiyo ilimpa Mama Kanje nguvu mpya, na akaanza kuweka akiba ya ziada kwa ajili ya kununua daftari na penseli za Sembo.

Mama Kanje alipata habari kwamba Acsa alikuwa ameanza kuwapatia watoto wake chakula kidogo zaidi baada ya kupata onyo kutoka kwa viongozi wa kijiji. Hii ilikuwa ushindi mdogo, lakini ilimpa matumaini kwamba watoto wake wangeweza kuishi kwa amani kidogo.

Aliketi chini ya kitanda, akachukua kalamu, na kuandika: “Mungu, nisaidie niwe mama hodari. Watoto wangu ni taa yangu.”

SURA YA SABA

Mama Kanje alihamia kabisa Bukoba, ambapo aliendelea na kazi yake ya ndani kwa Bi. Melisa.

Nyumba ya Bi. Melisa ilikuwa ya kisasa, na kulikuwa na umeme na maji ya bomba. Lakini maisha ya Mama Kanje bado yalikuwa magumu. Alifanya kazi kuanzia saa kumi alfajiri hadi saa sita usiku, akisafisha, kupika, na kufua nguo za watoto watatu wa Bi. Melisa.

Mara nyingi alipokea matusi kutoka kwa watoto wa Bi. Melisa, ambao walimwita “mtumishi” badala ya jina lake.

Lakini Mama Kanje alikuwa ameanza kujifunza jinsi ya kushinda maumivu ya maneno. Alikumbuka ushauri wa Mama Zawadi: “Usiruhusu maneno yakuvunje. Wewe ni zaidi ya mtumishi.” Alipata nguvu kutoka kwa maneno

hayo, na akaanza kuona kazi yake kama hatua ya kwanza kuelekea uhuru.

Aliongeza bidhaa zake za kuuza, akiuza sasa ndizi, mikeka, vikapu, na vitumbua. Biashara yake ilianza kukua, na akaanza kupata wateja wa kawaida, wengi wao wakiwa akina mama wa soko.

Siku moja, alipata fursa ya kushiriki katika soko la kila mwezi la Bukoba, ambapo wafanyabiashara wadogo walikuwa wakiuzia bidhaa zao. Alifuma mikeka kumi na mbili na vikapu vinne, na akauza karibu zote siku hiyo.

Pesa alizopata aliziweka akiba kwa ajili ya kununua sare za shule za Kanje na Sembo.

Alipata barua nyingine kutoka kijijini, ikisema kuwa Kanje alikuwa amefanikiwa kuingia darasa la sita, na Sembo alikuwa ameanza shule ya

msingi. Habari hizi zilimpa furaha kubwa, na alisema:

“Hata kama niko mbali, jasho langu linawafikia.”

******

Mama Kanje alianza kujiunga na kikundi cha akina mama wa Bukoba waliokuwa wakiweka akiba pamoja. Kikundi hicho kilimudu fursa ya kupata mikopo midogo ya kuongeza biashara yake.

Alichukua mkopo wa shilingi elfu hamsini na kununua vifaa vya kufuma mikeka zaidi.

Alifuma mikeka yenye miundo ya kipekee, ikiwa na rangi za kijani, manjano, na nyekundu, ambazo zilimpa wateja wengi zaidi. Biashara yake ilianza kumpa jina, na watu walianza kumuita “Mama Mikeka” sokoni.

Mama Kanje alipata changamoto mpya.

Bi. Melisa alimpa kazi za ziada, akisema kuwa Mama Kanje alikuwa “amezoea kazi ngumu.” Lakini Mama Kanje hakulalamika.

Alikumbuka maisha yake ya utotoni, alipokimbia vita, na alijua kuwa mateso ya sasa yalikuwa madogo ikilinganishwa na yale.

******

Wakati mwingine alipokuwa akipata likizo fupi kutoka Bukoba, Mama Kanje alikuja kuwaona. Lakini aliwekewa masharti:

“Ukija, hautaingia ndani. Watoto hawapo!” Acsa alikuwa akiwafungia kabisa watoto ndani na kuwafunika dirisha kwa mapazia mazito. Alihofia huruma ya mama yao ingezua shida kwake. Mara chache alipopata nafasi ya kuwaona, aliwakuta

wamekonda, wamedhoofika, wenye ngozi kavu na macho yenye huzuni.

Aliwalilia moyoni. Akawapa pipi ndogo na vitambaa vya kupangusa machozi.

“Mama yenu yupo. Msikate tamaa,” aliwaambia kwa sauti ya upole iliyojaa uzito wa mateso.

SURA YA NANE

Wakati Mama Kanje aliporudi nyumbani mara moja akiwa amependeza kidogo baada ya muda mrefu wa kazi, Baba Kanje alimtazama kwa macho tofauti. Akamwambia kwa sauti ya kujifanya mpole:

“Nilikosea sana… Naona umebadilika, mrembo kweli… Wanaume hulegea wakiona kama wewe. Rudi nyumbani... watoto wanakuhitaji.”

Maneno hayo yalikuwa ya hila. Mama Kanje aliwaza sana. Moyo wake ulimwambia asirudi, lakini watoto wake walimkumbuka. Aliamua kurejea. Baba Kanje alijenga haraka nyumba ndogo ya pili nyuma ya nyumba kuu.

Acsa akahamishiwa huko kwa manung’uniko. Mama Kanje akarudi katika nyumba yao ya awali.

Mwaka 2005, Mama Kanje alijifungua mtoto wa kiume – wakamwita Baraka. Kwa muda mfupi, walifurahia kama familia. Lakini haikudumu. Baba Kanje alirudia ulevi, uzinzi, na ukatili wake wa zamani.

Baba Kanje alionekana mara kwa mara akitembea na wanafunzi wa sekondari. Kilichoshtua kijiji kizima ni pale alipompa ujauzito binti wa kidato cha pili. Wazazi wa binti walitaka afungwe. Baba Kanje alitoroka usiku mmoja, akapotea kama upepo.

Mama Kanje alibaki na mzigo wa kulea watoto peke yake – bila pesa, bila msaada, bila matumaini akayarudia maisha ya zamani ya kulitegemea jembe na biashara ya ndizi ambayo ngiyo ilikuwa na soko.

Hakuwa anafuma mikeka tena wala vikapo kwakuwa hakukuwa na wateja wa kuwauzia kama ilivyokuwa Bukoba.

******

Kabla hata Baraka hajafikisha mwaka mmoja, nyumbani kwa Mama Kanje paligeuka kuwa gereza la mateso. Baba Kanje alirudi kutoka mafichoni, akavaa ngozi ya upole kwa muda mfupi, lakini haraka aligeuka kuwa yule yule – mlevi, mzinzi, na mkatili.

Sasa alikuwa na chuki zaidi, kana kwamba maisha yalikuwa yameharibu roho yake kabisa.

Mama Kanje, akiwa na watoto watatu sasa, alilazimika kufanya kazi za kilimo kwa bidii— mashamba ya viazi, mihogo, ndizi, na parachichi.

Hapo ndipo alipovuna na kuuza, akitumia kipato hicho kulisha watoto, kununua sare za shule, na kuwahudumia wanapougua. Baba Kanje alikuwa akinywa pombe ya gongo kila siku, akirudi usiku wa manane na kulala chumbani huku akinuka pombe na jasho la wanawake wa vichochoroni.

Siku moja, familia ya Baba Kanje ilifika ghafla kwa kikao. Walisema kuna taarifa kuwa Mama Kanje anataka kumweka sumu mumewe.

“Mimi nimemsikia kwa masikio yangu haya mawili akisema anataka aondoke kabisa ili usumbufu wake uishe,” alisema shemeji mmoja aliyekuwa kipenzi cha Acsa.

Bila ushahidi wowote, walimtazama Mama Kanje kwa macho ya hukumu, kama mtuhumiwa tayari aliyehukumiwa. Baba Kanje akasimama na kusema: “Huyu mwanamke sasa amefika mwisho

wake. Hatakiwi tena hapa.” Kanje alikuwa pembeni, akiwa amesimama na mama yake, huku macho yake yakiwa yamejaa hofu. Lakini kabla hajajitetea, Acsa alimvuta pembeni na kumwambia kwa sauti ya chini:

“Ukisema mama yako ni mchawi aliyepanga sumu, nitakununulia viatu na nguo mpya. Vinginevyo, utalala tena kwenye godoro la majani.”

Kanje, akiwa bado mtoto mdogo mwenye njaa ya upendo na vitu vizuri, akasaliti mama yake. Kwa sauti ya kutetemeka, alisema: “Mama alisema mara moja... ati angefurahi kama baba angekufa.”

Maneno hayo yaliwasha moto wa maamuzi haraka. Mama Kanje alitetemeka. Akalia kimya, machozi yakimdondoka kama mvua ya masika.

Hakujitetea, alinyamaza kwa uchungu wa maumivu ya kusalitiwa na mwanawe wa kwanza.

Baba Kanje alimpiga makofi mawili hadharani. “Hili ndio fundisho kwa wake wa kisasa. Ukiona mambo magumu, unaanza kupika sumu!” Alimtupia nguo zake nje kwa mara ya pili.

Mama Kanje alichukua mkoba wake wa plastiki uliotoboka alionunua huko Bukoba, akiwa amefungwa khanga moja tu aliyoinunua miaka miwili iliyopita.

Baraka, akiwa bado mdogo sana, mwenye miaka miwili na nusu tu alilia sana kuachwa na mama yake, “Sembo mwanangu hakikisha unamuangalia mdogo wako” Mama Kanje alimwambia Sembo huku machozi yakimtoka yeye Pamoja na Sembo.

Alihama kijiji usiku wa manane. Alitembea hadi Msumba kwa mzee John akaomba hifadhi ya siku moja, usiku huo aliutumia kupiga simu kwa Bi. Melisa akimuomba arudi kuwa mjakazi wake, lakini alimwambia kuwa hakuwa na nafasi tena ila akaahidi kumtafutia kazi kwa rafiki yake.

Bi. Melisa alimtafutia kazi ya ndani haraka sana kwa rafiki yake aliyekuwa akiishi jijini Dar es Salaam.

“Utapita kwanza huku Bukoba halafu nitakusaidia namna ya kufika Dar es Salaam” Bi. Melisa alimwambia Mama Kanje kupitia simu. Usiku wote Mama Kanje hakulala, hata hivyo Aliona ni neema hata kupata nafasi tena ya Kwenda kufanya kazi.

Kesho yake asubuhi mapema sana aliamka akaomba lifti kwenye gari ya mizigo lililokuwa

likienda Bukoba. Ndani ya gari kulikuwa na magunia ya maharage na ndizi, Mama Kanje akalala juu yake na baridi ilimkumbatia kama kifo, lakini hofu ya kurudi ilimlazimisha kuvumilia.

SURA YA TISA

Mama Kanje alihamia Dar es Salaam baada ya kupata fursa ya kazi ya ndani kwa familia ya mzungu na mkewe wa Kitanzania rafiki yake Bi. Melisa.

Alikuwa mtumishi wa familia ya watu wanne: baba mzungu, mama Mtanzania, na watoto wawili wa shule ya kimataifa. Alifua, alisafisha, alisafisha tena.

Mara nyingine hata chakula hakikuwa chake. Alipewa mabaki ya chakula cha watoto—chipsi zilizoisha chumvi, wali baridi, au vipande vya nyama vilivyoachwa kwenye sahani.

Lakini katika kila pumzi aliyoitoa, Mama Kanje aliwaza jambo moja: “Kila jasho langu ni mbegu kwa maisha bora ya watoto wangu.”

Maisha ya jiji yalikuwa tofauti kabisa na Karagwe na Bukoba. Maisha yalibadilika – kazi ilikuwa nyingi lakini angalau hakupigwa.

Alijifunza kupika vyakula vya kizungu, kufanya usafi kwa kutumia vifaa vya kisasa, na kuzungumza Kiingereza cha majumbani: “Clean the dishes, sweep the floor, feed the dog.”

Sauti za magari, vigelegele vya baa, na milio ya honi zilileta hisia ya upweke zaidi. Lakini Mama Kanje alikuwa na lengo moja: kuwapa watoto wake maisha bora.

Alifanya kazi kuanzia saa kumi alfajiri hadi saa tano usiku, akisafisha, kupika vyakula vya kizungu, na kuwalisha mbwa wa familia hiyo.

Nyumba aliyofanya kazi ilikuwa kubwa, na kulikuwa na vifaa vya kisasa kama mashine ya kufulia nguo na jiko la gesi. Lakini maisha yake

yalibaki kuwa magumu. Alipokea mshahara mdogo, ambao aliuweka akiba kwa ajili ya watoto wake.

Siku moja, alipokea barua kutoka kwa jirani kijijini, ikisema kuwa Kanje alikuwa ameanza kutoroka nyumbani kwa sababu ya mateso ya Maisha Magumu na kukosa chakula.

Sembo alikuwa ameugua homa ya matumbo, na hakuna aliyempatia dawa. Mama Kanje alilia usiku huo, lakini aliamua kuchukua hatua.

Alituma pesa zote alizokuwa ameweka akiba kwa jirani, akiomba ampeleke Sembo hospitali. Alikaa jikoni usiku huo, akapiga magoti akasali, na kusema:

"Mungu, usiwaruhusu watoto wangu wafe kabla ya kuwapa maisha bora."

Alipata wazo la kuuza vitumbua jioni baada ya kazi kwa siri kwani hakuruhusiwa kabisa kufanya biashara kama ilivokuwa Karagwe na Bukoba, aliwauzia walinzi wa geti na wauguzi wa zahanati karibu na nyumba.

Biashara hiyo ilimpa pesa za ziada, ambazo alizitumia kununua viatu vya shule kwa Sembo na kutuma hela ya chakula.

Alipata barua nyingine baadaye, ikisema kuwa Sembo alikuwa amepona, na Kanje alikuwa amerejea shuleni baada ya kupata msaada wa mwalimu wake wa zamani.

Mara kwa mara alijiuliza: “Kwa nini maisha yangu ni vita isiyoisha? Kwa nini kila hatua ya mbele lazima iwe na miiba?” Lakini hakujipa nafasi ya kujuta. Aliamua maisha yake yawe

daraja kwa watoto wake, japo yeye mwenyewe alitembea juu ya makali ya wembe.

Siku moja alipokuwa anafua, mtoto wa mwenye nyumba alimwambia:

"Wewe ni mtu mzuri. Mama yangu alisema unapambana sana."

Alitabasamu kwa uchungu. Alijua maisha yake yamesahauliwa na dunia, lakini bado kulikuwa na chembe ya heshima kwa jasho lake.

******

Kila alipokaa jioni akiwa peke yake jikoni, alikumbuka mateso aliyoyapitia. Alimkumbuka Kanje, aliyeishi kwa ukimya na hasira, na Sembo, aliyekuwa mwepesi wa kulia. Alijilaumu kwa kuwacha nyuma, hata kama ilibidi.

“Watasema mama yetu alitukimbia?” aliwaza mara kwa mara. Alijilaumu pia kwa kurudi kwa Baba Kanje. Alijua alipaswa kumsamehe tu kwa mioyo yao, si kwa kurudi kuishi naye. Lakini mahitaji ya watoto, kiu ya kuwaona tena, na udhaifu wa moyo wa mama ndivyo vilimrudisha kwenye moto ule ule.

Usiku mmoja, akiwa amechoka sana, Mama Kanje alipata maumivu makali ya tumbo. Alijua alikuwa akiumia kwa ndani—moyo, si tumbo. Alipumua kwa shida, lakini aliogopa kuomba msaada. Hakutaka afukuzwe.

Alilala sakafuni jikoni, karibu na chombo cha maji, huku Baraka akiwa kwenye picha ndogo mfukoni mwake. Picha hiyo ilikuwa ya mtoto aliyemchekesha kwenye giza, aliyempa sababu ya kupambana.

******

Kila alipoenda sokoni kununua mboga za nyumba ya bosi wake, aliona wanawake waliovaa vizuri, waliokuwa wakitembea kwa uhuru. Wengine walikuwa wajasiriamali, wengine walikuwa wanawake wa maofisini. Aliwaza:

"Mimi nitaendelea kuwa mtumishi hadi lini?" Aliamua jambo moja—atapambana. Hata kama dunia haitamuona, ataacha alama kwa watoto wake. Usiku mmoja, baada ya kumaliza kazi, alikaa sebuleni peke yake. Aliandika katika daftari lake dogo:

"Ninataka watoto wangu waje wajivunie mama yao. Hata kama nitakufa maskini, nataka wawe matajiri wa heshima, elimu na uzalendo." Aliweka daftari hilo chini ya godoro lake la

sakafu. Daftari hilo lilikuwa kama moyo wake wa pili.

Mama Kanje aliamua kuacha kazi ya ndani kwani alikuwa akipewa mshahara mdogo sana licha ya kazi nyingi za kuchosha, alitumia fedha alizokuwa nazo za ziada akakodi chumba kimoja cha giza na kisichokuwa na sakafu kule Mbagara jijini Dar es Salaam, akaanza kuishi peke yake kwa kujitegemea, hapo akawa huru tena kufanya biashara kwa nguvu zake zote.

Siku iliyofuata, alianza kutafuta kazi nyingine ya ziada. Aligundua kuwa jirani yao alikuwa na familia ya Wahindi waliotaka mtu wa kusafisha ofisi mara mbili kwa wiki. Alijitolea. Alipata elfu kumi kila usiku. Alianza kuweka akiba kidogo.

Mama Kanje alianza kujifunza kuhusu maisha ya jiji. Aligundua kuwa watu wa Dar es Salaam walikuwa na kasi ya maisha, lakini wengi walikuwa na mioyo mizuri. Alikutana na Mama Mbogo, mwanamke wa Kizaramo ambaye alikuwa na mgahawa mdogo.

Mama Mbogo alimshauri Mama Kanje afanye kazi ya ziada ya kupika maandazi na supu ya ng'ombe. Mama Kanje alikubali, na akaanza kufanya kazi hiyo kwa mtaji mdogo.

Mama Kanje alipata picha nyingine ya watoto wake, wakiwa wamesimama mbele ya shule yao. Alishika picha hiyo, akaitazama kwa muda mrefu, na kusema"Hii ni sababu yangu ya kuamka kila siku. Watoto wangu watajua kuwa mama yao hakuwaacha."

SURA YA KUMI

Wiki moja baadaye, alikutana na mama mmoja sokoni aliyekuwa akiuza vitambaa vya batiki na vitenge. Mama huyo alimwambia: “Natafuta mtu wa kuaminika wa kuuza vitambaa vyangu siku za Jumapili. Unaweza?” Kwa mara ya kwanza, macho ya Mama Kanje yaliangaza. Alikubali. Akaanza kuuza vitenge Jumapili kwa faida ndogo.

Sasa Mama Kanje alikuwa anafanya kazi sehemu tatu! Jumatatu na Jumatano alifanya usafi katika ofisi ya wahindi, Jumapili aliuza vitenge vya batiki na siku zilizobaki aliuza vitumbua na supu ya ng’ombe. Akaweza kupata fedha ya kutosha na kulipa kodi ya pango haikuwa shida tena.

Pesa hiyo aliitumia kununua viatu vya Kanje, Sembo na Baraka —viatu vya rangi ya Mama Kanje.

Katika kijiji cha mbali, Sembo na Kanje walikuwa bado wakihangaika. Acsa aliwatesa kimya kimya, akiwalazimisha kulima, kupika, na kufua nguo za watoto wake.

Lakini walikuwa wakijua kuwa mama yao anapambana. Kila walipopokea viatu, nguo, au vitafunwa kutoka mjini, walikuwa wanasema: “Mama yetu hajatuacha.”

Alipata habari kutoka kijijini kupitia simu ya Jirani yake, ikisema kuwa Kanje alikuwa ameingia darasa la saba, na Sembo alikuwa ameshinda tuzo nyingine ya uchoraji.

Walimu wao waliwapongeza kwa bidii na nidhamu. Kanje alianza kuongoza darasani, na Sembo akawa na kipaji cha uchoraji. Waligundua kuwa maumivu huzaa ubunifu.

Habari hizi zilimpa nguvu mpya, na akaanza kuweka akiba zaidi kwa ajili ya ada za shule.

Alikua mwanachama wa kikundi cha akina mama wa Mbagara, ambapo aliweza kupata mikopo midogo ya kuongeza biashara yake ya vitumbua na supu ya ng'ombe.

******

Mama Kanje alianza kugundua nguvu ya kujitegemea. Alianza kufuma mikeka na vikapu vya kipekee, na akaanza kupata jina sokoni kama "Mama Mikeka." Alipata wateja wa kawaida, wengi wao wakiwa akina mama waliopenda bidhaa zake za mikono.

Alipata barua nyingine kutoka kijijini, ikisema kuwa Kanje alikuwa ameanza kuandika hadithi fupi za maisha yao, na Sembo alikuwa amechora

picha ya mama yake akiwa amesimama chini ya mti wa mwembe.

Mama Kanje alikumbuka siku alipokimbia vita vya Rwanda, na alijua kuwa mateso yake ya sasa yalikuwa ni sehemu ya safari yake ya kumpa maisha bora.

Aliketi jikoni usiku mmoja, akachukua daftari lake dogo, na kuandika: “Mungu, nimeona giza nyingi, lakini sasa naona mwanga. Watoto wangu watanifanya niwe mama wa heshima.”

SURA YA KUMI NA MOJA

